



**KISII UNIVERSITY**  
**UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**THIRD YEAR EXAMINATION FOR THE AWARD OF THE**  
**DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION [ARTS]**  
**SECOND SEMESTER 2021/2022**  
**[JUNE-SEPTEMBER, 2022]**

**KISW 321: ORAL LITERATURE AND FIELD WORK IN KISWAHILI**

**STREAM: Y3S2**

**TIME: 2 HOURS**

**DAY: THURSDAY, 9:00 – 11:00 AM**

**DATE: 08/09/2022**

**MAAGIZO**

- 1. Usiandike chochote katika karatasi hii ya maswali.**
- 2. Jibu swali la KWANZA na mengine MAWILI.**

**SWALI LA KWANZA**

- a) Eleza kwa tafsili Mbinu zozote tano za ukusanyaji data nyanjani. (Alama 10)
- b) Bainisha mchango wa Nadharia ya *Ubadilikaji* na *Saiko-changanuzi* katika kueleza usuli wa fasihi Simulizi. (Alama 16)
- c) Fafanua sifa za *vivugo* na *tendi*. (Alama 4)

**SWALI LA PILI**

- a) Eleza sifa tano zinazotambulisha kila moja ya vipera vifuatavyo:
  - i) Mazungumzo. (Alama 5)
  - ii) Nyimbo. (Alama 5)
  - iii) Methali. (Alama 5)
- b) Fasihi Simulizi inatofautiana na fasihi andishi. Eleza ukitumia hoja tano. (Alama 5)

### **SWALI LA TATU**

- a) Kama mtafiti wa fasihi Simulizi, Eleza changamoto zozote tano unazotarajia nyanjani, na upendekeze suluhisho kwa kila changamoto. (Alama 15)
- b) Fafanua nafasi ya vipera vifuatavyo katika jamii za Kiafrika. (Alama 5)
  - i) Ngomezi.
  - ii) Hodiya.

### **SWALI LA NNE**

- a) Ukitumia mifano mwafaka, eleza dhamira ya matumizi ya takriri katika vipera vyovyote viwili vya fasihi simulizi. (Alama 10)
- b) Bainisha umuhimu wa dhana zifuatazo katika utafiti nyanjani.
  - i) Uteuzi wa sampuli mtabakisho.
  - ii) Kubainisha malengo na mipaka.
  - iii) Uchambuzi na ufasiri wa data. (Alama 10)

### **SWALI LA TANO**

“Katika karne ya ishirini na moja, fasihi Simulizi inaelekea kuzikwa katika kaburi la sahou” Eleza mambo yoyote sita yanayochangia hali hii. (Alama 20)